# Kiswahili curriculum design

## UTANGULIZI

***Umuhimu wa Somo la Kiswahili***

Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya. Ni lugha ya mawasiliano katika eneo la Afrika Mashariki na Kati. Wakenya wengi hujifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Ni muhimu wanafunzi wapate umilisi wa kuwasiliana kwa Kiswahili mapema hasa katika kiwango cha kwanza cha elimu. Aidha, somo la Kiswahili katika kiwango hiki humwandaa mwanafunzi kwa mafunzo ya viwango vya juu na baadaye katika ajira.

***Umilisi wa Kimsingi***

Mtaala mpya umejumuisha masuala tofauti na ambayo ni muhimu kwa kila mwanafunzi. Miongoni mwa masuala haya ni pamoja na umilisi wa kimsingi. Mtaala mpya umetambua umilisi tofauti ambao anapaswa kujengwa, mwanafunzi anapoendeleza masomo yake. Umilisi huu ni pamoja na:

- Mawasiliano na ushirikiano
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo
- Ubunifu
- Uraia
- Ujuzi wa kidijitali
- Hamu ya kuendelea kujifunza
- Kujiamini.

Inaaminika kwamba, mwanafunzi akipata umilisi ufaao, ataweza kufaa katika jamii inaobadilika kila uchao. Kutokana na imani hii, kazi katika mtaala huu imepunguzwa ili mwalimu apate nafasi murua kumsaidia mwanafunzi kujenga umilisi huu. Pamoja na haya, mtaala

umempa mwanafunzi nafasi kubwa ya kushiriki katika masimulizi, usomaji na kufanya kazi katika vikundi. Vilevile, vifaa vya kidigitali vimependekezwa katika kila mada.

***Maadili ya Kimsingi***

Pamoja na umilisi wa kimsingi ni maadili ya kimsingi. Jamii isiyokuwa na maadili ni jamii ambayo imejaa uozo. Maadili katika jamii yanahakikisha kuwa raia wanaishi vizuri na kunawiri katika kila nyanja. Mtaala umetaja maadili ya kimsingi yafuatayo:

- Mapenzi
- Heshima
- Uaminifu
- Uwajibikaji
- Uzalendo
- Haki za Kijamii
- Umoja
- Amani.

Maadili haya yametokana na katiba ya Kenya na yanadhamiriwa kujumuishwa katika kila kipindi na kila somo. Hii ndiyo njia mwafaka ya kuhakikisha kuwa watoto na vijana wetu wametayarishwa kuwa raia waadilifu baada ya maisha shuleni.

***Masuala Mtambuko***

Haya ni masuala muhimu na ambayo mwanafunzi anatakiwa kuyaelewa na kujua jinsi ya kuyakabili katika maisha ya kila siku. Licha ya mtalaa kuhusisha masuala, masuala zaidi yaweza kujitokeza darasani. Mwalimu ahakikishe kuwa anayasisitiza anapoendelea na shughuli zake darasani. Akumbuke kuwa mbinu atakazozijumuisha katika kufundisha zaweza kuimarisha msisitizo wa masuala haya au zikakwamiza juhudi zilizowekwa kuhakikisha kwamba masuala haya hayapuuzwi. Miongoni mwa masuala yanayolengwa katika mtalaa ni pamoja na uwazi, kushirikisha wazazi katika masomo, uwazi, usalama, lishe bora na afya na elimu ya maendeleo endelevu.

***Uhusiano na Masomo Mengine***

Ni wazi kuwa, kila mada katika somo lolote huwa na uhusiano na mada nyingine katika masomo tofauti. Mtalaa huu umeundwa kwa njia ambapo mwalimu na mwanafunzi wataweza kurejelea masomo mengine na hivyo kujenga umilisi unaodhamiriwa kwa njia bora zaidi.

Vilevile, kusisitiza uhusiano huu kunadhamiriwa kuangazia umuhimu wa ushirikiano wa wanafunzi wanaonawiri katika masomo tofauti na pia walimu wanaofunza masomo husika kwa lengo moja tu ambalo ni kufaulisha elimu.

***Uhusiano na Shughuli za Huduma kwa Kijamii Zinazochangia Ujifunzaji***

Kila somo sharti liwe na maana kwa mwanafunzi. Umuhimu wa mada yoyote ndio chanzo cha umakinifu darasani. Sababu kuu ya kusisitiza umilisi wa kimsingi ni kuhakikisha kwamba kuna uhusiano kati ya kinachofunzwa shuleni na maisha ya kila siku nje na ndani ya shule. Kutokana na hayo, katika kila mada, mapendekezo yametolewa ya jinsi mwanafunzi anaweza kuhamisha alichojifunza darasani hadi nyumbani. Ni muhimu uhusiano huu usisitizwe ili kuonyesha maana na umuhimu wa elimu.

***Uhusiano na Shughuli Zingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji***

Ni wazi kuwa mwanafunzi hujifunza kutokana na shughuli tofauti tofauti ndani ya darasa na nje ya darasa. Kuna shughuli nyingi ambazo huchangia pakubwa katika ujifunzaji. Mtalaa mpya umeongeza msisitizo wa shughuli hizi kutoka na umuhimu wake katika kufaulisha ujifunzaji. Shughuli hizi ni pamoja na vikundi vya ushirika shuleni, michezo ya kuigiza, kukariri na kuimba mashairi miongoni mwa mengine. Ni muhimu wanafunzi wahusishwe katika shughuli hizi ambazo kwazo zitachangia pakubwa katika kufaulisha shughuli za ujifunzaji.

***Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini***

Mfumo mpya wa elimu unadhamiria kuhakikisha kuwa matokeo ya mafunzo ni ujenzi wa umilisi utakaomwezesha mwanafunzi kutumia ujuzi wake kujiendeleza. Kutokana na hayo, mfumo huu unadhamiria kupunguza usisitizo wa mtihani wa mwisho wa viwango mbalimbali. Inatarajiwa kuwa mwanafunzi ataendelea kutathminiwa huku akiendelea kupata mafunzo zaidi. Mtalaa huu umependekeza mfumo wa kukadiria kiwango cha mwanafunzi. Mwanafunzi hatakuwa akilinganishwa na wenzake bali uwezo wake utakadiriwa kulingana na viwango vilivyopendekezwa. Kigezo hiki kimeorodhesha viwango vinne katika kukadiria uwezo wa mwanafunzi: anayezidisha matarajio; anayefikia matarajio; anayekaribia matarajio na aliye mbali na matarajio. Inatarajiwa kuwa mwalimu atajaribu mbinu tofauti baada ya tathmini yoyote ile kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanafikia matarajio kwa mujibu wa matokeo maalum yanayotarajiwa katika kila mada.

***Jinsi Mtalaa huu Ulivyopangwa***

Mtalaa huu umejumuisha stadi zote zinazofaa kufunzwa katika gredi ya kwanza, ya pili na ya tatu. Lugha yoyote ile ina stadi nne ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Inajulikana wazi kwamba, ili anayejifunza lugha aweze kupata umilisi ufaao, stadi hizi sharti zifunzwe pamoja. Hata hivyo, kwa vile wanafunzi wengi wanaingia shuleni bila kujua lugha ya Kiswahili, imeamuliwa kuwa wanafunzi wa gredi ya kwanza wasifunzwe kusoma na kuandika katika muhula wa kwanza ili kujenga umilisi wa kusikiliza na kuzungumza kwanza. Utafiti umeonyesha wazi kwamba mtu anapoelewa kuzungumza lugha yoyote ile, inakuwa rahisi kwa mtu yuyo huyo kusoma na kuandika katika lugha husika. Kutokana na haya, mtalaa huu imepangwa kwa kutumia mada zilizochaguliwa kwa msingi ya kimaudhui. Kila gredi imetengewa mada zake. Kila mada nayo ina mada ndogo kadhaa ambazo zimejikita katika stadi nne za lugha pamoja na msamiati na sarufi. Inatarajiwa kuwa, kadri inavyowezekana, yatakayojumuishwa katika kila mada ndogo yajikite katika maudhui lengwa.

***Kusikiliza na Kuzungumza***

Stadi hii inalenga mawasiliano kwa kutumia mdomo. Ili kujenga stadi hii, ni muhimu mwanafunzi kushirikishwa katika mazungumzo. Miongoni mwa mada zinazolenga mazungumzo ni pamoja na maamkizi, maagizo, msamiati, maagano, masimulizi na maelezo. Katika kuelekeza wanafunzi katika mada hizi, mwalimu anatakiwa kumpa mwanafunzi nafasi ya kujieleza, ashirikishwe katika maigizo na mijadala darasani. Ikumbukwe kuwa, kila neno analotamka mwanafunzi linachangia katika kujenga umilisi wa lugha. Mwalimu asilenge wanafunzi wanaochukuliwa kuwa werevu darasani tu. Licha ya mada ya kusoma kushirikishwa katika muhula wa kwanza, mada hii inadhamiriwa kujenga umilisi wa kusikiliza miongoni mwa wanafunzi. Mwanafunzi anaposikiliza hadithi ikisomwa, ataweza kuanza kuthamini usomaji. Hata hivyo, mjadala atakaoshirikishwa baada ya kusikiliza hadithi ikisomwa na mwalimu utamsaidia kuanza kuwa makini na vilevile kumpa nafasi ya kutumia Kiswahili katika mazungumzo.

***Kusoma***

Katika kila mada ya hadithi baada ya muhula wa kwanza gredi ya kwanza, mwanafunzi anatakiwa kusikiliza hadithi ikisomwa na mwalimu na vile vile kuna hadithi yake ambayo ataongozwa na mwalimu kusoma. Wakati mwalimu anaposoma hadithi na ambayo haitakuwa katika kitabu cha mwanafunzi, mwalimu anatakiwa kujua kuwa jinsi anavyosoma ndivyo mwanafunzi wake atakavyosoma baadaye. Ni muhimu kufanya mazoezi ya kutosha ili kuimarisha matamshi na ufasaha. Lazima ahakikishe kuwa kasi katika kusoma kwake ni ya kadri ili kuwafaa mwanafunzi katika kiwango chake. Mwalimu ahakikishe kwamba anamhusisha mwanafunzi katika hadithi yake kwa kumwongoza kujadili msamiati, picha, kutabiri, kuthibitisha utabiri na kuwauliza maswali anapoendelea kusoma. Ili kupima kiwango cha ufahamu wa mwanafunzi, mwalimu anatarajiwa kuwa atawauliza maswali baada ya kusoma na vilevile kumpa nafasi kutoa muhtasari wa hadithi na kujadili mafunzo katika hadithi.

***Kuandika***

Stadi ya kuandika ni muhimu katika mawasiliano. Kuzungumza na kuandika ndizo stadi mbili zinazomwezesha mwanafuzi kuwasiliana na wengine. Mazungumzo hufaa tu mzungumziwa anapokuwa karibu au kupitia mbinu za kiteknolojia kama vile simu. Stadi hii kwa hivyo ni muhimu katika mawasiliano na mtu aliye mbali kupitia kwa barua ya kawaida au barua pepe pamoja na kuweka kumbukumbu mambo muhimu. Umilisi wa kuandika umeanza kujengwa katika gredi ya kwanza muhula wa pili. Stadi hii imejikita katika mada za sauti, msamiati, majibu ya maswali ya hadithi katika maandishi na sarufi ambayo, pamoja na kujadiliwa darasani, inapendekezwa kwamba mazoezi ya kisarufi yaandikwe katika madaftari ya wanafunzi. Inakisiwa kuwa mwanafunzi afikapo katika gredi ya tatu, atakuwa na umilisi wa kutosha wa kuanza kuandika visa vifupi kutegemea mada inayolengwa.

Gredi ya tatu vilevile imejumuisha hatua tano za uandishi kama njia ya kumwelekeza mwanafunzi katika kuijenga stadi ya uandishi. Hatua hizi ni: maandalizi, nakala ya kwanza, marejeleo, uhariri na uchapishaji. Hatua hizi zinadhamiriwa kuhakikisha kuwa mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika kila hatu na hivyo kuweza kuandika kisa kifupi na sentensi chache haraka iwezekanavyo. Mwanafunzi anapofikia kiwango cha uchapishaji ambapo utungo wake unaweza kupachikwa kwenye ukuta kwa kila mwanafunzi kuusoma, atakuwa ameanza kujiamini katika utunzi. Utunzi unaofuata hatua hizi waweza kufunzwa kama kazi mradi.

***Msamiati***

Msamiati ni idadi ya maneno katika lugha. Msamiati humsaidia mwanafunzi katika kujenga hazina yake ya maneno anayoweza kutumia katika mawasiliano. Katika mtalaa huu, kila mada kuu ina msamiati unaohusiana nayo. Mwalimu ahusishe mwanafunzi katika kujifunza matumizi ya msamiati unaolengwa. Ikumbukwe kuwa, lengo si kutaja idadi kubwa ya maneno darasani. Mwalimu alenge kuhakikisha kuwa mwanafunzi amepata umilisi wa kutumia neno lililofunzwa katika mawasiliano ya kila siku. Zifuatazo ni hatua zinazofaa katika kufunza msamiati:

- Onyesha neno unalofunza
- Muulize mwanafunzi iwapo amewahi kulisikia neno hilo
- Iwapo amewahi kulisikia, muulize iwapo anajua maana
- Toa maana ya neno kwa kuigiza, kuonyehsa picha au kifaa halisi, kutumia neno lingine rahisi lenye maana sawa na neno unalolenga au kufafanua maana kwa maneno mepesi ya kiwango cha mwanafunzi
- Tumia neno lengwa katika sentensi ili mwanafunzi aweze kujua maana kimktadha
- Mshirikishe mwanafunzi katika kutunga sentensi akitumia neno lengwa

Yafaa ieleweke kuwa kadri inavyowezekana, mada ya msamiati inafunzwa kabla ya masimulizi na hadithi ili kuhakikisha kuwa mwanafunzi anayaelewa maana ya maneno husika kabla hajahusishwa katika kusoma au masimulizi. Jambo hili linampa mwanafunzi nafasi murua ya kutumia msamiati aliojifunza katika muktadha halisi.

***Sauti na Majina ya Herufi za Kiswahili***

Ni wazi kuwa binadamu amezungumza kwa miaka mingi zaidi ikilinganishwa na miaka ambayo binadamu amekuwa akisoma na kuandika. Kutokana na hayo, ni muhimu kutilia mkazo sauti. Umilisi katika kutamka sauti utamsaidia mwanafunzi kuwasiliana katika mazungumzo kwa urahisi. Utafiti umeonyesha kwamba, zipo sauti ambazo jamii husika hutumia mara nyingi katika mazungumzo na maandishi. Kwa mfano, watoto wengi kuanza kwa kutamka sauti **/m/** kwa kuwa neno **mama** huwa ndilo neno la kwanza kutamkwa miongoni mwa jamii nyingi zinazotumia Kiswahili nchini. Kutokana na haya, pendekezo lililotolewa la utaratibu wa kujifunza sauti na herufi umetokana na umuhimu na wingi wa matumizi ya sauti lengwa katika mawasiliano. Hili litamwezesha mwanafunzi kuweza kusoma kwa haraka kwa vile sauti na herufi anayofunzwa mwanzo ni ile ameizoea katika mazungumzo. Mpangilio wa jinsi sauti zinavyofunzwa usichukuliwe kuwa kama njia ya kupuuza alfabeti kama tunavyoijua. Mpangilio huu ni wa kumwezesha mwanafunzi kuzungumza na kusoma mapema. Alfabeti imeingizwa baadaye mwanafunzi anapojitayarisha kuanza kutumia kamusi. Sauti na herufi hizi zimepangwa katika makundi matatu. Makundi haya ni:

- sauti zinazowakilishwa na herufi moja
- sauti zinazowakilishwa na herufi mbili
- sauti mbili zinazotamkwa pamoja katika neno

Katika kufunza sauti hizi, mwanafunzi ataelekezwa kuzisikiliza, kuzitamka, kuzitambua katika maneno, kuandika herufi zinazoziwakilisha na pia kufanyishwa mazoezi ya kuzitamka sauti hizo anaposikiliza na kusoma hadithi yenye maneno yanayozijumuisha. Katika kufunza sauti, mwalimu ahakikishe kuwa amezitamka sauti hizo kwa usahihi. Kwa vile kila binadamu ana upungufu wake, mwalimu asione haya kumwalika mwalimu mwenzake au mgeni darasani kumsaidia kutamka sauti zinazomtatiza. Vifaa vya kiteknolojia vilivyo na sauti zilizohifadhiwa vilevile vitamsaidia kuzisikiliza sauti lengwa na kuzitamka ipasavyo ili kumfaidi mwanafunzi anayemtagemea kwa matamshi bora.

***Sarufi***

Sarufi inahusu matumizi ya lugha. Kila lugha ina sheria zinazoitawala. Ni kutokana na sheria hizi ambapo kila mzungumzaji wa lugha anaweza kujua anapotumia lugha vilivyo na anapotumia lugha kimakosa. Mtalaa umeundwa kwa njia ambayo mwanafunzi atajifunza sarufi katika muktadha wa matumizi. Vilevile, sarufi katika kiwango hiki imepunguzwa na kupewa vipindi vitakavyomwezesha mwanafunzi kufanya mazoezi zaidi kwa lengo la kujenga umilisi ufaao. Miongoni mwa vipengee vya sarufi vilivyojumuishwa ni pamoja na nafsi, nyakati na ukanusho, viashiria, vivumishi, vinyume, umoja na wingi.

***Matokeo ya Kijumla Yanayotarajiwa Katika Kiwango cha Kwanza cha Masomo***

Kufikia mwisho wa kiwango cha kwanza cha masomo, mwanafunzi aweze:

a. Kutumia mbinu zifaazo za usikivu katika mawasiliano kwenye mazingira yake
b. Kudhihirisha ufasaha wa kuzungumza kwa kiswahili
c. Kusoma kwa ufasaha na kufahamu aina zozote za maandishi ya kiswahili
d. Kuelezea mawazo, hisia na tajiriba kwa maandishi ya mkono au mbinu nyingine yoyote ya uwasilishaji
e. Kutumia sarufi ipasavyo katika mawasiliano
f. Kutumia msamiati ufaao katika mazingira yake kuwasiliana
g. Kuonyesha ukakamavu katika kuwasilis

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Karibu Darasani** | Kusikiliza na Kuzungumza: Maamkuzi (Vipindi 3) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kutambua maneno yatumiwayo katika maamkuzi<br>b. Kuamkua na kuitikia maamkuzi ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>c. Kutambua umuhimu wa salamu katika mawasiliano<br>d. Kufurahia kushiriki katika maamkuzi. | • Mwanafunzi aigize maamkuzi kama vile hujambo? Sijambo; Hamjambo? Hatujambo darasani<br>• Mwanafunzi ajadili mchoro wa watu wawili wakisalimiana<br>• Wanafunzi wasalimiana na kisha washirikishwe katika mjadala kuhusu maamkuzi<br>• Wanafunzi waweza kuwekwa katika vikundi ili wajadili kuhusu umuhimu wa maamkuzi<br>• Wanafunzi wawili waweza kushirikishwa katika kuigiza maamkuzi mepesi<br>• Wanafunzi waweza kuigiza maamkuzi darasani wakiwa wawili wawili | **1) Tunatumia maneno gani katika salamu?**<br>**2) Tunatakiwa kusalimiana vipi?**<br>**3) Kwa nini tunasalimiana?** |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Maagizo (Vipindi 2) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kutambua maagizo mepesi yanapotolewa darasani<br>b. Kutoa na kufuata maagizo mepesi yanayotumiwa darasani<br>c. Kubainisha maagizo yanayopaswa kufuatwa katika mazingira yake<br>d. Kuthamini umuhimu wa maagizo katika maisha ya kila | • Mwanafunzi ashiriki katika kutoa na kufuata maagizo kama vile simama, keti, andika na chora<br>• Mwanafunzi aweza kuonyeshwa video ya jinsi ya kutoa na kufuata maagizo<br>• Mwanafunzi ashiriki katika mjadala wa maagizo yafaayo na yasiyofaa kufuatwa<br>• Mwanafunzi afafanue umuhimu wa maagizo<br>• Mwanafunzi aweza kushirikishwa katika masimulizi ya matokeo ya kufuata na kutofuata | **1) Umewahi kuambiwa ufanye jambo lolote?**<br>**2) Ni nani anayetakiwa kutoa maagizo?**<br>**3) Ni maagizo yepi yanayotakiwa kufuatwa na yasiyotakiwa** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | siku. | maagizo<br>• Mwanafunzi aweza kushirikishwa katika kuimba nyimbo na kukariri mashairi yanayohusu maagizo | **kufuatwa?**<br>**4) Kufuata maagizo kuna umuhimu gani?** |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Msamiati (Vipindi 2) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kutambua kwa majina vifaa vinavyopatikana darasani ili kurahisisha mawasiliano<br>b. Kutumia majina ya vifaa vya darasani katika sentensi ili kuwezesha mazungumzo<br>c. Kufurahia kutumia na kutunza vifaa vinavyopatikana darasani. | • Mwanafunzi ataje vifaa halisi k.v. dawati, kitabu, kalamu na kifutio<br>• Mwanafunzi aweza kuonyeshwa picha za vifaa halisi na kutaja majina<br>• Mwanafunzi achore maumbo ya vifaa vya darasani<br>• Wanafunzi waweza kuambatanisha kadi za maneno na vifaa halisi darasani wakiwa katika vikundi.<br>• Mwanafunzi ajibizane na mwenzake kuhusu vifaa vya darasani k.m. Hii ni nini? Hii ni kalamu. | **1) Je, wajua vitu unavyotumia darasani?**<br>**2) Je, wajua umoja na wingi wa vitu vya darasani?** |
| | Kusoma: Hadithi (Vipindi 3) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;**<br>a. Kutambua msamiati uliotumika katika hadithi ili kuimarisha ufahamu<br>b. Kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu ili kujenga usikivu<br>c. Kufahamu hadithi aliyosomewa darasani katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>d. Kuchangamkia hadithi katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusomewa hadithi<br>• Mwanafunzi aeleze matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi<br>• Mwanafunzi aulize na kujibu maswali.<br>• Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu hadithi wakiwa wawili wawili<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ikisomwa kwa kutumia tarakilishi na projekta | **1) Kwa nini unapenda picha?**<br>**2) Unapenda hadithi?**<br>**3) Kwa nini unapenda hadithi?**<br>**4) Unakumbuka hadithi uliyosikiliza?** |
| | | | | |

| | |
|---|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**<br>Mawasiliano na ushirikiano – Wutumie lugha faafu katika mazingira ya darasani na washiriki katika kazi ya vikundi<br>Ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza | |
| **Uhusiano na masuala mtambuko:** Uraia: Utangamano wa kijamii; wanafunzi watangamana wanapoamkuana na kufanya kazi pamoja | **Uhusiano na maadili:** Heshima na adabu |
| **Uhusiano na masomo mengine:** English Activities, Literacy and Indigenous Languages | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:** Kuwaelezea wengine umuhimu wa kwenda shuleni. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>Uigizaji wa maamkuzi<br>Kazi ya vikundi | **Mapendekezo ya tathmini:**<br>Kuchunguza mwanafunzi anavyoamkua na kupokea maamkuzi. Kuchunguza jinsi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi. |

## Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| ***Mwanafunzi,***<br>• anaamkua na kuitikia maamkuzi ifaavyo<br>• anafuata maagizo kwa makini na kutoa maagizo kwa lugha sanifu<br>• anatumia msamiati aliofunzwa kwa ubunifu katika mawasiliano<br>• anafahamu hadithi na masimulizi aliyosimuliwa kwa wepesi. | ***Mwanafunzi,***<br>• anaamkua na kuitikia maamkuzi ifaavyo<br>• anafuata maagizo na kutoa maagizo kwa lugha sanifu<br>• anatumia msamiati aliofunzwa katika mawasiliano<br>• anafahamu hadithi na masimulizi aliyosimuliwa. | ***Mwanafunzi,***<br>• anaamkua na kuitikia maamkuzi ifaavyo<br>• anafuata maagizo lakini ana changamoto katika kutoa maagizo kwa lugha sanifu<br>• ana changamoto katika kutumia baadhi ya msamiati aliofunzwa katika mawasiliano<br>• anafahamu baadhi ya hadithi na masimulizi aliyosimuliwa. | ***Mwanafunzi,***<br>• anaamkua na kuitikia baadhi ya maamkuzi<br>• anafuata baadhi ya maagizo lakini ana changamoto katika kutoa maagizo<br>• ana changamoto katika kutumia msamiati aliofunzwa katika mawasiliano<br>• ana changamoto katika kufahamu hadithi na masimulizi aliyosimuliwa. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Mimi na Wenzangu** | Kusikiliza na Kuzungumza: Maelezo (Vipindi 3) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br><br>a. Kutambua wenzake darasani kwa majina, jinsia, miaka na gredi ili kuweza kuwaelezea<br>b. Kujieleza kwa kurejelea jina, jinsia, miaka na gredi kwa ufasaha katika mawasiliano ya kila siku<br>c. Kutoa muhtasari wa maelezo aliyoyasikia katika mazingira yake<br>d. Kudhihirisha umakinifu wa kusikiliza katika mazingira yake<br>e. Kuchangamkia maelezo yake na ya wenzake katika kuimarisha mawasiliano<br>f. Kujivunia nafsi yake na wenzake katika miktadha mbalimbali. | • Mwanafunzi asikilize maelezo ya wengine.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza maelezo ya wenzake yaliyorekodiwa kwenye simu, kinasa sauti, kipatakalishi n.k.<br>• Wanafunzi watoleane maelezo kuwahusu katika vikundi.<br>• Wanafunzi wakiwa wawili wawili waulizane. maswali na kujibizana k.m. Unaitwaje?<br>• Mwanafunzi atoe maelezo yake akizingatia jina, jinsia, umri na gredi mbele ya darasa.<br>• Mwanafunzi aeleze maana ya msamiati unaotumiwa kujieleza k.v. umri, miaka,msichana, mvulana, gredi na rafiki.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi kwa kutumia maneno yanayotumiwa kujieleza na kueleza wenzake.<br>• Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu maana na matumizi ya msamiati unaotumiwa k.m. umri, miaka, msichana, mvulana, gredi na rafiki katika vikundi. | **1) Wewe ni nani?**<br>**2) Mwenzako ni nani?**<br>**3) Unapenda kufanya nini?** |
| | Kusikiliza na | **Kufikia mwisho wa mada,** | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2) | **mwanafunzi aweze:**<br><br>a. Kusimulia hadithi aliyosikiliza darasani ili kujenga stadi ya kusikiliza<br>b. Kufahamu hadithi aliyosimuliwa ili kupata ujumbe<br>c. Kuonyesha umakinifu wa kusikiliza katika miktadha mbalimbali<br>d. Kuchangamkia hadithi simulizi maishani. | • Mwanafunzi aweze kuwa makini anaposimuliwa masimulizi.<br>• Mwanafunzi asikilize masimulizi kupitia vifaa vya kiteknolojia k.m. simu, kinasa sauti, kipatakalishi n.k.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza mgeni mwalikwa akisimulia masimulizi.<br>• Wanafunzi waweza kuwekwa katika vikundi na kutoleana muhtasari wa masimulizi yaliyosimulia.<br>• Mwanafunzi aulize na kujibu maswali kutokana na masimulizi. | **1) Umewahi kusimuliwa kisa kipi?**<br>**2) Unatarajiwa kufanya nini unaposimuliwa masimulizi?**<br>**3) Unakumbuka nini katika masimulizi uliyosimuliwa?** |
| | Kusoma: Hadithi (Vipindi 3) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br><br>a. Kutambua msamiati uliyotumika katika hadithi ili kuweza kuutumia katika mawasiliano<br>b. Kusikiliza hadithi zikisomwa ili kujenga usikivu<br>c. Kufahamu hadithi aliyosomewa darasani ili kupata ujumbe<br>d. Kuchangamkia kusikiliza hadithi kila siku. | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusomewa hadithi.<br>• Mwanafunzi aeleze matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Wanafunzi wajadiliane kuhusu hadithi waliosomewa katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kushirikishwa kusikiliza hadithi zikisomwa kupitia vifaa vya teknolojia k.v. tarakilishi, projekta n.k.<br>• Mwanafunzi aweza kuonyeshwa picha na kadi za msamiati uliotumiwa katika hadithi.<br>• Mwanafunzi aulize na kujibu maswali | **1) Je, ni hadithi kusomewa?**<br>**2) Unatarajiwa kufanya nini unaposomewa hadithi?**<br>**3) Unakumbuka nini katika hadithi uliyosomewa?**<br>**4) Unafikiria ni nini kitakachotokea katika hadithi hii?** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kutokana na hadithi | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**
Mawasiliano na ushirikiano – Wanatumia lugha faafu katika kujieleza darasani. Vilevile wanashiriki katika kazi ya vikundi
Ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko:** Stadi za maisha: kujitambua na kujithamini kijamii wanapojieleza | **Uhusiano na Maadili:** Heshima kwa wengine |
| **Uhusiano na masomo mengine:** English Activities, Literacy and Indigenous Languages, Religious Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>kujizatiti kuwajua wenzake shuleni na vijijini<br>kuwafunzi wenzake umuhimu wa kuwajua watu kwa majina kwa usalama wao. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>kazi ya vikundi<br>shughuli za vikundi vya ushirika shuleni. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>kuchunguza ukakamavu wa mwanafunzi anapojieleza kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi. |

## Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| ***Mwanafunzi,***<br>• Anajieleza kwa ukakamavu na ufasaha<br>• Anaelezea wenzake kwa ukakamavu na ufasaha<br>• Anasimulia kisa kwa lugha ifaayo na yenye ubunifu<br>• Anajibu maswali ya ufahamu wa hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi | ***Mwanafunzi,***<br>• Anajieleza kwa ufasaha<br>• Anaelezea wenzake kwa ufasaha<br>• Anasimulia kisa kwa lugha ifaayo<br>• Anajibu maswali ya ufahamu kwa usahihi<br>• Anatoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa. | ***Mwanafunzi,***<br>• Anajieleza ifaavyo<br>• Anaelezea wenzake ifaavyo<br>• Anasimulia baadhi ya visa<br>• Ana changamoto za kujibu baadhi maswali kutokana na hadithi<br>• Ana changamoto za kutoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa. | ***Mwanafunzi,***<br>• Ana changamoto za kujieleza ifaavyo<br>• Ana changamoto za kuelezeawenzake ifaavyo<br>• Ana changamoto katika kusimulia kisa<br>• Ana changamoto za kujibu maswali mengi kutokana na hadithi<br>• Ana changamoto za kutoa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| • Anatoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa kwa ubunifu. | | | muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Tarakimu** | Kusikiliza na Kuzungumza:Msamiati<br>(Vipindi 3) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kutambua nambari moja hadi kumi (1-10) katika mazingira yake<br>b. Kuhesabu nambari 1-10 kwa mfuatano ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>c. Kutaja majina ya nambari moja hadi kumi kwa mfululizo ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>d. Kutumia majina ya nambari moja hadi kumi kutunga sentensi ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>e. Kuthamini matumizi ya nambari katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi anaweza kupewa kadi za nambari azitaje kwa maneno.<br>• Mwanafunzi aweza kukariri mashairi kuhusu nambari hadi kumi.<br>• Mwanafunzi aweza kushirikishwa kuimba nyimbo za tarakimu.<br>• Wanafunzi waambatanishe nambari na maneno kwa kuonyeshwa nambari na kutaja jina la nambari husika.<br>• Wanafunzi wahesabu vidole kwa Kiswahili wakiwa wawili wawili k.m. mmoja anachukua kidole kimoja na mwingine anataja jina la nambari, ‘moja’ n.k.<br>• Wanafunzi wanaweza kupanga kadi za majina ya nambari hadi kumi kwa utaratibu.<br>• Mwanafunzi aweza kuonyeshwa nambari na jina kwa kutumia tarakilishi na projekta. | **1) Unajua kuhesabu nambari ngapi?**<br>**2) Hesabu moja hadi kumi.**<br>**3) Unaweza kutumia majina yapi ya nambari moja hadi kumi katika sentensi?**<br>**4) Ni nini umuhimu wa nambari maishani?** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aweza kuonyeshwa video ya wanafunzi wakisoma nambari hadi kumi kwa tarakilishi. | |
| | Kusikiliza na Kuzungumza:Masimulizi<br>(Vipindi 2) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br><br>a. Kusikiliza visa vinavyohusiana na nambari ili kujenga umakinifu<br>b. Kufahamu masimulizi ya visa vinavyohusiana na nambari ili kupata ujumbe<br>c. Kuonyesha umakinifu wa kusikiliza katika mawasiliano<br>d. Kuchangamkia masimulizi katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi asikilize kisa kikisimuliwa.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika kusimulia kisa kinachohusisha nambari.<br>• Mwanafunzi atoe muhtasari wa matukio yaliyosimuliwa.<br>• Wanafunzi waweza kusimuliana visa vinavyojumuisha nambari wakiwa wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza masimulizi kupitia kwa vyombo vya kiteknolojia kama vile simu, kinasasauti na kipatakalishi vyaweza kutumiwa katika kusimulia visa mbalimbali. | **1) Nambari hutumiwaje?**<br>**2) Unatarajiwa kufanya nini unaposimuliwa kisa?**<br>**3) Unakumbuka nini katika kisa ulichosimuliwa?** |
| | Kusoma:<br>Hadithi<br>(Vipindi 3) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;**<br><br>a. Kutambua msamiati uliotumika katika kurahisisha ufahamu<br>b. Kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu ili kujenga stadi ya kusikiliza<br>c. Kufahamu hadithi aliyosomewa ili kupata ujumbe<br>d. Kuchangamkia kusikiliza hadithi kila siku ili kujenga ari ya kusoma baadaye. | • Mwanafunzi ashirikiane na wengine kujadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma hadithi.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi akitumia msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Wanafunzi wajadiliane kuhusu hadithi waliosomewa katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi | **1) Umewahi kusikiliza hadithi ipi?**<br>**2) Unatarajiwa kufanya nini unaposomewa hadithi?**<br>**3) Kwa nini unapenda picha?**<br>**4) Unaweza kutabiri kitakachotokea** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | zikisomwa kupitia vifaa vya kiteknolojia k.v. tarakilishi, projekta n.k.<br>• Mwanafunzi aulize na kujibu maswali kutokana na hadithi. | **katika hadithi?**<br>**5) Unakumbuka hadithi uliyosomewa?** |

| | |
|---|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**<br>Mawasiliano na ushirikiano – Wanatumia lugha faafu darasani. Vilevile wanashiriki katika kazi ya vikundi<br>Ujuzi wa kidijitali – matumizi ya teknolojia katika kujifunza<br>Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi atapata hamu ya kuendelea kuhesabu kwa kutumia Kiswahili | |
| **Uhusiano na masuala mtambuko:** Stadi za maisha: kujitambua wanapohesabu viungo vya mwili. | **Uhusiano na Maadili:**<br>uwajibikaji wa kutunza alicho nacho na cha wenzake. |
| **Uhusiano na masomo mengine:** Mathematics Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>kutumia ujuzi wa kuhesabu katika biashara hasa anapotumwa dukani au sokoni. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>kazi ya vikundi<br>shughuli za vikundi vya ushirika shuleni<br>michezo. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>kuchunguza uwezo wa kuhesabu kwa Kiswahili<br>kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa. |

## Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| ***Mwanafunzi ,***<br>• Ana hesabu moja hadi kumi kwa haraka<br>• Anatumia msamiati wa nambari kwa ubunifu katika sentensi<br>• Anasimulia kisa kwa ufasaha na | ***Mwanafunzi ,***<br>• Anahesabu moja hadi kumi<br>• Anatumia msamiati wa nambari katika sentensi ifaavyo | ***Mwanafunzi ,***<br>• Ana changamoto chache hesabu moja hadi kumi<br>• Ana changamoto za kutumia baadhi ya msamiati wa nambari katika sentensi | ***Mwanafunzi ,***<br>• Ana changamoto nyingi katika kuhesabu moja hadi kumi<br>• Ana changamoto za kutumia msamiati wa nambari katika sentensi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| ubunifu<br>• Anajibu maswali ya ufahamu hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi<br>• Anatoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa au kusomewa kwa ubunifu. | • Anasimulia kisa kwa ufasaha.<br>• Anajibu maswali ya ufahamu hadithi na masimulizi kwa usahihi<br>• Anatoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa au kusomewa. | • Anasimulia baadhi ya visa<br>• Ana changamoto za kujibu baadhi ya maswali ya ufahamu wa hadithi na masimulizi<br>• Anatoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa au kusomewa. | • Ana changamoto katika kusimulia kisa<br>• Ana changamoto za kujibu maswali mengi kutokana na hadithi na masimulizi<br>• Ana changamoto za kutoa muhtasari wa hadithi aliyosimuliwa au kusomewa |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Siku za wiki** | Kusikiliza na Kuzungumza: Msamiati<br>*(Vipindi 3)* | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kutambua siku za wiki katika mawasiliano ya kila siku<br>b. Kutaja majina ya siku za wiki kwa mfululizo ili kumsaidia kuratibu shughuli za siku<br>c. Kuelezea shughuli za siku mbalimbali za wiki ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>d. Kutumia majina ya siku za wiki kutunga sentensi ili kuimarisha mawasiliano<br>e. Kuthamini kila siku ya wiki ili kutilia maanani shughuli za siku husika maishani. | • Mwanafunzi atambue siku za wiki yaani: Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alhamisi, Ijumaa, Jumamosi na Jumapili kwa kutumia kadi za maneno.<br>• Mwanafunzi aweza kuimba wimbo wa siku za wiki.<br>• Mwanafunzi aweza kukariri mashairi kuhusu siku za wiki.<br>• Mwanafunzi ashiriki katika majadiliano ya shughuli za siku za wiki k.m. Jumatatu naenda shule, Ijumaa, Jumamosi au Jumapili nashiriki ibada n.k.<br>• Wanafunzi waweza kupanga kadi za majina ya siku za wiki kwa utaratibu wakiwa wawili wawili. | **1) Wiki moja ina siku ngapi?**<br>**2) Unaenda shule siku gani?**<br>**3) Unaweza kutaja na kuandika majina yapi ya siku za wiki kwa mfuatano?**<br>**4) Waweza kutumia majina yapi ya siku za wiki katika sentensi?** |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:** | • Mwanafunzi asimulie kisa darasani. | **1) Ni matukio** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Masimulizi<br>*(Vipindi 2)* | a. Kusimulia matukio katika siku tofauti za wiki ili kujenga stadi ya kuzungumza<br>b. Kufahamu masimulizi ya matukio ya siku za wiki aliyosimuliwa ili kupata ujumbe<br>c. Kuonyesha umakinifu wa kusikiliza katika mawasiliano<br>d. Kuchangamkia masimulizi maishani ili kuimarisha usikivu. | • Mwanafunzi aonyeshe umakinifu anaposikiliza masimulizi ya mwalimu na wanafunzi wenzake.<br>• Wanafunzi waweza kusimuliana matukio ya siku za wiki wakiwa wawili wawili.<br>• Mwanafunzi asikilize masimulizi kuhusu matukio ya siku za wiki kupitia vifaa vya kiteknolojia k.m. simu, kinasasauti, kipakatalishi n.k.<br>• Wanafunzi waweza kuwekwa katika vikundi na kutoleana muhtasari wa matukio yaliyosimuliwa hasa kwa kutumia vifaa vya teknolojia.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali kutokana na masimulizi aliyosikiliza. | **yapi uliyowahi kushuhudia?**<br>**2) Unatarajiwa kufanya nini unaposimuliwa kisa?**<br>**3) Unakumbuka nini katika matukio uliyosimuliwa?** |
| | Kusoma Hadithi<br>*(Vipindi 3)* | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kutambua msamiati uliotumika katika hadithi ili kuimarisha ufahamu<br>b. Kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu zinazojumuisha matukio ya siku za wiki ili kujenga umakinifu<br>c. Kufahamu hadithi aliyosomewa katika mada ili kupata ujumbe<br>d. Kuchangamkia kusikiliza hadithi kila siku. | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusomewa hadithi.<br>• Mwanafunzi asikilize hadithi ikisomwa na mwalimu.<br>• Mwanafunzi aeleze matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Wanafunzi waweza kujadiliana kuhusu hadithi waliyosomewa katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kushirikishwa kusikiliza hadithi kwa kutumia vifaa vya teknolojia k.v. tarakilishi, projekta n.k.<br>• Mwanafunzi aweza kuonyeshwa picha na | **1) Umewahi kusikiliza hadithi ipi?**<br>**2) Unatarajiwa kufanya nini unaposomewa hadithi?**<br>**3) Unafikiri ni nini kitakachotokea katika hadithi?**<br>**4) Unakumbuka hadithi ipi uliyosomewa?** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kadi za maneno yaliyotumiwa katika hadithi.<br>• Mwanafunzi ajibu na aulize maswali kutokana na hadithi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**
Mawasiliano na ushirikiano – kazi za vikundi
Ujuzi wa kidijitali : kuandika kwa vipakatalishi
Ubunifu: kueleza namna ya kutumia kila siku aliyo nayo.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>stadi za Maisha (uwajibikaji) -kufanya uamuzi wa jinsi ya kutumia siku za wiki<br>uzalendo: kushirikiana katika vikundi. | **Uhusiano na Maadili:**<br>heshima kwa siku zilizotengewa shughuli za kidini |
| **Uhusiano na Masomo mengine:** Literacy activities na Mathematics Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>kusisitiza umuhimu wa shughuli tofauti kwa mfano siku za kwenda shule, siku ya kupumzika na siku ya kwenda maabadini kwa wenzake na miongoni mwa wanajamii. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>kazi ya vikundi<br>shughuli za vikundi vya ushirika shuleni<br>michezo. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br> kuchunguza jinsi anavyoorodhesha siku za wiki na kuzitungia sentensi<br> kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa. |

## Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| *Mwanafunzi,*<br>• Anaorodhesha siku za wiki | *Mwanafunzi,*<br>• Anaorodhesha siku za | *Mwanafunzi,*<br>• Ana changamoto katika | *Mwanafunzi,*<br>• Ana changamoto nyingi katika |

| | | | |
|---|---|---|---|
| kwa haraka na ifaavyo<br>• Anatumia majina ya siku za wiki katika mawasiliano kwa ubunifu<br>• Anasimulia kisa kwa ufasaha na ubunifu<br>• Anajibu maswali ya ufahamu hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi. | wiki ifaavyo<br>• Anatumia majina ya siku za wiki katika mawasiliano<br>• Anasimulia kisa kwa ufasaha<br>• Anajibu maswali ya ufahamu hadithi na masimulizi kwa usahihi. | orodhesha siku za wiki ifaavyo<br>• Ana changamoto za kutumia majina ya siku za wiki katika mawasiliano<br>• Anasimulia baadhi ya visa<br>• Anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi. | kuorodhesha siku za wiki<br>• Ana changamoto nyingi katika kutumia majina ya siku za wiki katika mawasiliano<br>• Ana changamoto katika kusimulia visa<br>• Ana changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu hadithi na masimulizi. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Familia** | Sauti na majina ya herufi za Kiswahili *(Vipindi 8)* | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br><br>a. Kutamka sauti nne za herufi moja ili kuimarisha mazungumzo<br>b. Kutambua sauti za herufi moja zilizofunzwa katika maneno ili kuimarisha mazungumzo<br>c. Kutambua majina ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>d. Kusoma herufi za sauti moja katika kujenga stadi ya kusoma<br>e. Kusoma maneno kwa kutumia | • Mwanafunzi ashirikishwe kutambua sauti /m/, /a/, /u/ na /k katika maneno.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu akitamka sauti lengwa, kisha watamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili na katika darasa.<br>• Mwanafunzi atumie teknolojia (papaya) kutamkia sauti.<br>• Mwanafunzi atambue herufi inayowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi.<br>• Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno.<br>• Wanafunzi waweza kushirikishwa kusikiliza mgeni mwalikwa mwenye umahiri wa kutamka sauti lengwa. | **1) Ni sauti zipi unazojua kutamka?**<br>**2) Unajua kusoma herufi na maneno yapi?**<br>**3) Unajua kuandika herufi na maneno yapi?** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | silabi zinazotokana na sauti lengwa katika kujenga stadi ya kusoma<br>f. Kusoma vifungu vilivyo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kujenga stadi ya kusoma<br>g. Kuandika maumbo ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kuandika<br>h. Kuchangamkia kutumia maneno yanayojumuisha sauti zilizofunzwa katika mawasiliano ya kila siku. | • Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi au kugawa maneno marefu zaidi vipande vipande.<br>• Wanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa kama darasa au wawili wawili.<br>• Mwanafunzi asikilize na kusoma hadithi kupitia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta n.k.<br>• Mwanafunzi afinyange na aandike maumbo ya herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni.<br>• Mwanafunzi aandike maneno yaliyo na herufi za sauti alizofunzwa kwa kunakili aliyoandika mwalimu. | |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Maneno ya heshima *(Vipindi 2)* | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kutambua maneno ya heshima katika familia<br>b. Kutumia maneno ya heshima katika mawasiliano<br>c. Kuambatanisha maneno ya heshima na hisia zifaazo katika mawasiliano<br>d. Kuthamini matumizi ya maneno ya heshima katika mawasiliano ya kila siku. | • Wanafunzi waweza kuonyeshwa mchoro wa mtoto akipokea zawadi halafu wajadili neno linalofaa kutumiwa na anayepokea zawadi.<br>• Mwanafunzi aweza kuonyeshwa video inayoashiria matumizi ya maneno ya heshima k.m. Mtu akipokea zawadi au wageni wakimtembelea mgonjwa hospitalini.<br>• Mwanafunzi aweza kupewa ufafanuzi kuhusu maneno ya heshima kama vile “asante, pole na tafadhali.”<br>• Wanafunzi waweza kushirikishwa katika kuigiza vitendo vya heshima.<br>• Mwanafunzi ahusishwe katika mjadala kuhusu umuhimu wa kutumia maneno ya heshima. | **1) Unapopewa zawadi unatakiwa kusema nini?**<br>**2) Mwenzako anapojikwaa utamwambiaje?**<br>**3) Unapoomba ruhusu kutoka kwa mwalimu unatumia neno gani?** |
| | Kusoma: | **Kufikia mwisho wa mada,** | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Hadithi<br>*(Vipindi 4)* | **mwanafunzi aweze:**<br><br>a. Kutambua msamiati uliotumika katika hadithi<br>b. Kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu zinazohusu familia darasani<br>c. Kusoma hadithi kuhusu familia darasani<br>d. Kufahamu hadithi aliyosomewa kuhusu familia darasani<br>e. Kuchangamkia kusikiliza hadithi kila siku. | • Mwanafunzi aweza kujadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi aweza kutabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi aweza kufuatilia hadithi ikisomwa na mwalimu, kisha asome pamoja na mwalimu na baadaye asome akiwa peke yake au wiwili wawili.<br>• Mwanafunzi aweza kueleza maana na matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi ukiwemo msamiati wa familia kama vile baba, mama, kaka na dada.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza mwalimu anaposoma hadithi, asome pamoja na mwalimu na kisha asome peke yake, wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi asikilize hadithi ya mwalimu au iliyorekodiwa inayojumuisha matumizi ya maneno ya heshima.<br>• Mwanafunzi aweza kutoa muhtasari wa hadithi aliyosoma au aliyosomewa.<br>• Wanafunzi waweza kutunga sentensi wakitumia majina ya watu wa familia katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia jitabu mbele ya darasa.<br>• Mwanafunzi aweza kuthibitisha utabiri wake baada ya kusomewa hadithi.<br>• Wanafunzi waweza kushirikishwa katika | **1) Unatakiwa kufanya nini unaposomewa hadithi?**<br>**2) Unakumbuka nini katika hadithi uliyosomewa?**<br>**3) Unaweza kutabiri kitakachotokea katika hadithi?**<br>**4) Unaweza kusoma hadithi?**<br>**5) Kwa nini unapenda hadithi?**<br>**6) Unakumbuka hadithi gani uliyosoma?** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuuliza na kujibu maswali kutokana na hadithi darasani na vilevile kuyaandika kwenye madaftari yao. | |
| | Sarufi: Nafsi ya kwanza wakati uliopo *(Vipindi 3)* | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kutambua maneno na viambishi vinavyotumika kuonyesha nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi katika sentensi<br>b. Kusoma vifungu vya maneno vinavyoashiria nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi<br>c. Kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi katika sentensi<br>d. Kuandika vifungu vya maneno vinavyoashiria nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi<br>e. Kufurahia kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi katika mawasiliano. | • Mwanafunzi aweza kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi katika mawasiliano.<br>• Mwanafunzi aweza kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi katika sentensi.<br>• Manafunzi aweza kusoma sentensi zinazojumuisha matumizi ya nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi.<br>• Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia maneno na viambishi vinavyowakilisha nafsi ya kwanza na wakati uliopo kama vile; **mimi** ni**na** ; **sisi** tu**na**.<br>• Wanafunzi waweza kuigiza nafsi ya kwanza wakati uliopo hali ya umoja na wingi katika vikundi kwa kutumia vifungu kama vile mimi ninaandika-sisi tunaandika, mimi ninasoma-sisi tunasoma baadaye waongozwe kuandika vifungu hivi kwenye madaftari yao.<br>• Mwanafunzi aweza kupewa zoezi katika tarakilishi ili atumie mbinu ya kuburura majibu sahihi na kutia kapuni. | **1) Je, unatumia maneno gani kujirejelea na mkiwa wengi?**<br>**2) Ukiwa unafanya lolote sasa, utasemaje?** |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – Kujadiliana kuhusu majukumu ya watu wa familia; Kufanya kazi kwa vikundi
- Hamu ya ujifunzaji: Matumizi ya nafsi ya kwanza wakati uliopo
- Ujuzi wa kidijitali :Kuna mapendekezo ya kutumia vifaa vya teknolojia kufunzia
- Ubunifu: Utunzi wa sentensi kwa kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>• Uraia: uzalendo: kushirikiana katika vikundi<br>• Utangamano wa kijamii - mahusiano katika familia. | **Mahusiano na Maadili: M**apenzi katika familia. |
| **Uhusiano na masomo mengine:** Religious Studies, English Activities and Environmental Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>kutembelea nyumba ya mayatima na kucheza nao<br>kuwaelimisha wengine umuhimu wa familia katika ujenzi wa jamii. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>kazi ya vikundi<br>shughuli za vikundi vya ushirika shuleni<br>michezo. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• kuchunguza jinsi anavyowatambua watu katika familia yake<br>• kuchunguza anavyotamka sauti zilizofunzwa<br>• kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa<br>• kuchunguza jinsi anavyotumia nafsi ya kwanza wakati uliopo katika sentensi. |

## Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| ***Mwanafunzi,***<br>• Anawataja watu wa familia zaidi ya aliyofunzwa<br>• Anatumia majina ya watu wa familia kwa ubunifu katika sentensi<br>• Anasoma hadithi kwa ufasaha<br>• Anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi<br>• Anatumia nafsi ya kwanza wakati uliopo kutunga | ***Mwanafunzi,***<br>• Anawataja watu wa familia<br>• Anatumia majina ya watu wa familia katika sentensi ifaavyo<br>• Anasoma hadithi<br>• Anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi<br>• Anatumia nafsi ya kwanza wakati uliopo kutunga sentensi ifaavyo | ***Mwanafunzi,***<br>• Anawataja watu wa familia<br>• Anatumia majina ya watu wa familia katika sentensi<br>• Anasoma baadhi ya kazi anazopewa<br>• Anajibu baadhi maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi<br>• Ana changamoto za kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo kutunga sentensi | ***Mwanafunzi,***<br>• Anawataja watu wa familia<br>• Ana changamoto za kutumia majina ya watu wa familia katika sentensi<br>• Ana changamoto katika kusoma<br>• Ana changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu hadithi na masimulizi kwa usahihi<br>• Ana changamoto za kutumia nafsi ya kwanza wakati uliopo kutunga sentensi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| sentensi zenye ubunifu<br>• Anaandika kwa hati nadhifu. | • Anaandika kwa hati inayosomeka. | • Anaandika kwa hati inayosomeka. | • Ana changamoto katika kuandika |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Mwili Wangu** | Sauti na majina ya herufi za Kiswahili<br>*(Vipindi 8)* | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kutamka sauti nne za herufi moja katika kuimarisha mazungumzo<br>b. Kutambua sauti za herufi moja zilizofunzwa katika maneno<br>c. Kutambua majina ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>d. Kusoma herufi za sauti moja katika kujenga stadi ya kusoma<br>e. Kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa katika kujenga stadi ya kusoma<br>f. Kusoma vifungu vilivyo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kujenga stadi ya kusoma<br>g. Kuandika maumbo ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika | • Mwanafunzi atambue sauti /t/, /l/, /n/ na /o/ katika maneno.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu anapotamka sauti lengwa, kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili au kama darasa.<br>• Mwanafunzi atumie teknolojia (papaya) kutamkia sauti.<br>• Mwanafunzi atambue herufi inayowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi.<br>• Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno.<br>• Wanafunzi waweza kushirikishwa kusikiliza mgeni mwalikwa mwenye umahiri wa kutamka sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi na kuchanganua yaliyo marefu zaidi. | **1) Ni sauti zipi unazojua kutamka?**<br>**2) Unajua kusoma herufi na maneno?**<br>**3) Unajua kuandika herufi na maneno?** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kuimarisha stadi ya kuandika<br>h. Kuchangamkia kutumia maneno yanayojumuisha sauti zilizofunzwa katika mawasiliano ya kila siku. | • Wanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa kama darasa au wawili wawili.<br>• Mwanafunzi asikilize na kusoma hadithi kupitia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta n.k.<br>• Mwanafunzi afinyange na aandike maumbo ya herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni.<br>• Mwanafunzi aandike maneno yaliyo na herufi za sauti alizofunzwa kwa kunakili aliyoandika mwalimu. | |
| | Msamiati<br>*(Vipindi 3)* | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br><br>a. Kutambua sehemu za mwili katika mawasiliano<br>b. Kutumia majina ya sehemu za mwili katika kutunga sentensi<br>c. Kusoma majina ya sehemu za mwili katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>d. Kuandika majina ya sehemu za mwili katika kuimarisha stadi ya kuandika<br>e. Kuchangamkia utunzaji wa sehemu za mwili katika kuimarisha afya. | • Mwanafunzi aambanitishe kadi za maneno na sehemu za mwili za nje.<br>• Mwanafunzi aweza kuonyeshwa video kuhusu sehemu za mwili za nje.<br>• Mwanafunzi achore sehemu za mwili za nje.<br>• Mwanafunzi afafanue maana ya msamiati wa sehemu za mwili.<br>• Mwanafunzi asome hadithi baada ya mwalimu, kisha pamoja na mwalimu na baadaye akiwa peke yake au wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aweza kushirikishwa katika kuimba nyimbo na kukariri mashairi yanayohusu sehemu za mwili za nje.<br>• Mwanafunzi aandike majina ya sehemu za mwili za nje.<br>• Mwanafunzi atunge sentensi kuhusu sehemu za mwili za nje. | **1) Ni sehemu gani ya mwili unayoweza kuchora?**<br>**2) Sehemu tofauti za mwili za nje zina umuhimu gani?** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi achorewe sehemu za mwili kwenye tarakilishi ili atumie mbinu ya kuburura na kuweka kapuni ili kujazia mapengo. | |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi *(Vipindi 2)* | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kutambua sehemu za mwili katika mawasiliano<br>b. Kueleza matumizi ya sehemu za mwili ili kuthamini mwili wake<br>c. Kusimulia visa kuhusu sehemu za mwili katika kujenga stadi ya kuzungumza<br>d. Kuthamini sehemu za mwili wake maishani. | • Mwanafunzi ataje sehemu za mwili za nje.<br>• Mwanafunzi achore picha za sehemu mbalimbali za mwili za nje.<br>• Wanafunzi wajadili sehemu za mwili za nje na umuhimu wake katika vikundi.<br>• Mwanafunzi atoe maelezo kuhusu sehemu za mwili za nje.<br>• Mwanafunzi azungumzie sehemu zake za mwili za nje.<br>• Mwanafunzi aweza kuimba nyimbo na kukariri mashairi mepesi kuhusu sehemu za mwili za nje. | **1) Kuna sehemu ngapi za mwili za nje?**<br>**2) Sehemu za mwili za nje hutumiwa kufanya nini?**<br>**3) Ni sehemu ipi ya mwili ya nje iliyo muhimu zaidi?** |
| | Sarufi: Umoja na wingi wa majina *(Vipindi 3)* | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kutambua majina ya sehemu za mwili katika umoja na wingi ili kuimarisha mawasiliano<br>b. Kutumia majina ya sehemu za mwili kwenye sentensi katika umoja na wingi ili kuimarisha mawasiliano<br>c. Kusoma sentensi zinazojumuisha sehemu za mwili katika umoja na wingi ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>d. Kuandika sentensi zinazojumuisha sehemu za mwili katika umoja na | • Mwanafunzi atunge sentensi kwa kurejelea sehemu za mwili katika umoja na wingi.<br>• Mwanafunzi asome sentensi zinazorejelea sehemu za mwili katika umoja na wingi.<br>• Mwanafunzi aandike sentensi zinazorejelea sehemu za mwili katika umoja na wingi.<br>• Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia majina ya sehemu za mwili katika umoja na wingi.<br>• Mwanafunzi aweza kunakili sentensi katika umoja na wingi.<br>• Wanafunzi watunge sentensi katika umoja na wingi kwa vikundi. | **1) Je, ni sehemu gani za mwili unazoweza kutaja katika umoja na wingi?**<br>**2) Je, waweza kutumia majina gani ya sehemu za mwili katika sentensi?** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | wingi ili kuimarisha stadi ya kuandika<br>e. Kufurahia kurejelea sehemu za mwili katika umoja na wingi katika mawasiliano. | | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
Mawasiliano na ushirikiano – kupanga kujadiliana umuhimu wa sehemu za mwili; Kufanya kazi kwa vikundi
Hamu ya ujifunzaji: hamu ya kutaka kujua vitu vingine katika umoja na wingi
Ujuzi wa kidijitali :kuna mapendekezo ya kutumia vifaa vya teknolojia kufunzia
Ubunifu: utunzi wa sentensi katika umoja na wingi.

| | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko na Maadili:**<br>Stadi za maisha – kujitambua na kujithamini anapotaja sehemu zake za mwili; kujionea fahari kwa maumbile yake<br>Uraia: utangamano wa kijamii - kushirikiana katika vikundi. | **Uhusiano na maadili:**<br>Uwajibikaji<br>Mapenzi kwa mwili wake. |
| **Uhusiano na Masomo mengine:**<br>English Activities, Environmental Activities na Religious Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>Kusisitiza kuhusu utunzaji wa mwili miongoni mwa wenzake<br>Kulinda usiri wa mwili wake. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>Kazi ya vikundi<br>Shughuli za vikundi vya ushirika shuleni<br>Michezo. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• Kuchunguza jinsi anavyotambua sehemu mbalimbali za mwili<br>• Kuchunguza anavyotamka sauti zilizofunzwa<br>• Kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa<br>• Kuchunguza jinsi anavyotumia umoja na wingi wa majina katika sentensi. |

## Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| ***Mwanafunzi,*** <br>• Anatamka sauti lengwa ifaavyo na kwa ukakamavu <br>• Anaelezea sehemu lengwa za mwili ifaavyo <br>• Anatumia majina ya sehemu lengwa za mwili kwa ubunifu katika sentensi <br>• Anasoma kwa ufasaha <br>• Anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi <br>• Anatumia umoja na wingi wa majina lengwa katika kutunga sentensi ifaavyo kila wakati <br>• Anaandika kwa hati nadhifu na kwa haraka. | ***Mwanafunzi,*** <br>• Anatamka sauti lengwa vyema <br>• Anataja sehemu lengwa za mwili ifaavyo <br>• Anatumia majina ya sehemu lengwa za mwili ifaavyo katika sentensi <br>• Anasoma ifaavyo <br>• Anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi <br>• Anatumia umoja na wingi wa majina lengwa katika kutunga sentensi ifaavyo <br>• Anaandika kwa hati bora. | ***Mwanafunzi,*** <br>• Ana changamoto za kutamka baadhi ya sauti lengwa <br>• Anataja sehemu lengwa za mwili <br>• Ana changamoto za kutumia baadhi ya majina ya sehemu lengwa za mwili ifaavyo katika sentensi <br>• Anasoma baadhi ya kazi anazopewa <br>• Anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi <br>• Ana changamoto za kutumia umoja na wingi wa baadhi ya majina lengwa kutunga sentensi <br>• Anaandika kwa hati zinazosomeka. | ***Mwanafunzi,*** <br>• Ana changamoto za kutamka sauti lengwa <br>• Ana changamoto za kutaja baadhi ya sehemu lengwa za mwili <br>• Ana changamoto katika kusoma <br>• Ana changamoto za kutumia majina ya sehemu lengwa za mwili ifaavyo katika sentensi <br>• Ana changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi <br>• Ana changamoto za kutumia umoja na wingi wa majina lengwa kutunga sentensi <br>• Ana changamoto katika kuandika**.** |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Usafi wa Mwili** | Sauti na majina ya herufi za Kiswahili (Vipindi 8) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:** <br>a. Kutamka sauti nne za herufi moja katika kuimarisha mazungumzo | • Mwanafunzi atambue sauti /w/, /e/, /i/ na /h/ katika maneno. <br>• Mwanafunzi amsikilize mwalimu akitamka sauti | **1) Ni sauti zipi unazojua kutamka?** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | b. Kutambua sauti za herufi moja zilizofunzwa katika maneno ili kuimarisha mazungumzo<br>c. Kutambua majina ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>d. Kusoma herufi za sauti moja katika kujenga stadi ya kusoma<br>e. Kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa katika kujenga stadi ya kusoma<br>f. Kusoma vifungu vilivyo na maneno yaliyo na sauti lengwa ili kujenga stadi ya kusoma<br>g. Kuandika maumbo ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kuandika<br>h. Kuchangamkia kutumia maneno yanayojumuisha sauti zilizofunzwa katika mawasiliano ya kila siku. | lengwa, kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili wawili wawili na kama darasa.<br>• Mwanafunzi atumie teknolojia (papaya) kusikiliza matamshi ya sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi.<br>• Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno.<br>• Wanafunzi waweza kusikiliza mgeni mwalikwa mwenye umahiri wa kutamka sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi afinyange maumbo ya herufi za sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi aandike maumbo ya herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni.<br>• Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi na kuchanganua yaliyo marefu zaidi.<br>• Wanafunzi waweza kusoma hadithi zilizo na maneno yaliyobeba sauti lengwa kama darasa au wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza na kusoma hadithi kupitia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta n.k.<br>• Mwanafunzi aandike imla ya maneno yaliyo na herufi za sauti alizofunzwa na kuyaandika. | **2) Unajua kusoma herufi na maneno yapi?**<br>**3) Unajua kuandika herufi na maneno yapi?** |
| | Msamiati (Vipindi 2) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br><br>a. Kutambua msamiati wa usafi wa | • Mwanafunzi atambue msamiati wa usafi wa mwili k.m. kukata kucha, kunyoa nywele, kusafisha nguo, kusugua meno, kunawa mikono, | **1) Je, kwa nini unapenda kukaa ukiwa safi?**<br>**2) Ni vitendo vipi** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | mwili katika kujenga msamiati kwa mawasiliano<br>b. Kueleza maana ya msamiati wa usafi wa mwili ili kuimarisha mawasiliano<br>c. Kusoma msamiati wa usafi wa mwili katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>d. Kutumia msamiati wa usafi wa mwili katika sentensi<br>e. Kuandika maneno yanayohusiana na usafi wa mwili katika kuimarisha stadi ya kuandika<br>f. Kuthamini usafi wa mwili katika maisha ya kila siku. | kuoga na kufuta kamasi.<br>• Mwanafunzi atumie msamiati uliyofunzwa katika sentensi sahihi.<br>• Mwanafunzi aandike maneno yaliyofunzwa<br>• Mwanafunzi aweza kupewa kadi za maneno asome kwa sauti.<br>• Wanafunzi waweza kuambatanisha maneno waliofunzwa na michoro.<br>• Wanafunzi waweza kuimba nyimbo na kukariri mashairi kuhusu usafi wa mwili.<br>• Wanafunzi waweza kuwekwa katika vikundi wajadiliane kuhusu usafi wa mwili.<br>• Wanafunzi waweza kutazama video kuhusu vitendo tofauti vya usafi wa mwili. | **vinavyotusaidia kukaa tukiwa safi?** |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kutambua sehemu za mwili zinazopaswa kuangaziwa zaidi katika usafi katika kuimarisha mazungumzo<br>b. Kusikiliza hadithi kuhusu usafi wa mwili katika kurejelea stadi ya kusikiliza<br>c. Kufahamu masimulizi aliyoyasikiliza katika kurejelea stadi ya kusikiliza<br>d. Kusimulia visa vinavyohusu usafi katika kurejelea stadi ya kuzungumza | • Mwanafunzi asimuliwe hadithi kuhusu usafi kisha ashiriki katika mjadala kuhusu usafi wa mwili.<br>• Wanafunzi wasimuliane visa kuhusu usafi.<br>• Wanafunzi wajadiliane kuhusu sehemu za mwili zinazopaswa kuangaziwa zaidi katika usafi.<br>• Wanafunzi wajadiliana kuhusu umuhimu wa usafi maishani.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza mgeni mwalikwa k.m daktari au nesi akizungumzia juu ya usafi.<br>• Mwanafunzi ajibu na kuuliza maswali ya hadithi na maelezo aliyosikia kuhusu usafi.<br>• Mwanafunzi aweza kuhusishwa katika kuimba | **1) Je, ni sehemu zipi za mwili zinazopaswa kuangaziwa zaidi katika usafi?**<br>**2) Je, usafi una umuhimu gani?**<br>**3) Je, unaweza kusimulia kisa** kuhusu usafi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | e. Kufurahia masimulizi kuhusu usafi kila wakati katika mawasiliano. | nyimbo na kukariri mashairi kuhusu usafi wakiigiza vitendo vya usafi.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza nyimbo na mashairi yaliyorekodiwa kwenye vifaa vya kiteknolojia. | |
| | Kusoma: Hadithi (Vipindi 3) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. kutambua msamiati uliotumiwa katika hadithi ili kuimarisha mawasiliano<br>b. kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu zinazohusu usafi wa mwili katika kujenga stadi ya kusoma<br>c. kusoma hadithi zinazohusu usafi wa mwili katika kujenga stadi ya kusoma<br>d. kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa kuhusu usafi wa mwili ili kuimarisha mawasiliano<br>e. kudumisha usafi katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma na kusomewa hadithi.<br>• Mwanafunzi asome hadithi baada ya mwalimu, kisha pamoja na mwalimu na baadaye akiwa peke yake au wawili wawili.<br>• Mwanafunzi aeleze maana na matumizi ya msamiati uliotumika kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu anaposoma hadithi, asome pamoja na mwalimu kisha asome peke yake.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza hadithi ya mwalimu au hadithi iliyorekodiwa kuhusu usafi.<br>• Wanafunzi waweza kusomeana hadithi wakiwa wawili wawili na katika vikundi.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kupitia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta n.k. | **1) Je, ni nini maana ya usafi gani?**<br>**2) Je, ni matayarisho yapi unayofanya kabla ya kuja shuleni?**<br>**3) Unafikiri ni nini kitakachotokea katika hadithi hii?**<br>**4) Je, ni hadithi gani umewahi kusoma?** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi asome maneno yanayohusu usafi kwenye kadi.<br>• Mwanafunzi aweza kuhusishwa katika kuigiza vitendo vinavyohusu usafi wa mwili.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia jitabu mbele ya darasa.<br>• Mwanafunzi aweza kuonyeshwa picha zinazoashiria vitendo vya usafi wa mwili.<br>• Mwanafunzi aulize na kujibu maswali kutokana na hadithi. | |
| | Sarufi:<br>Matumizi ya **huyu** na **hawa**<br>(Vipindi 2) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br><br>a. Kutambua matumizi ya **huyu** na **hawa** katika mawasiliano<br>b. Kusoma sentensi zinazojumuisha **huyu** na **hawa** ili kuimarisha mawasiliano<br>c. Kutumia **huyu** na **hawa** katika sentensi katika kuimarisha mawasiliano<br>d. Kuandika sentensi kwa kutumia **huyu** na **hawa** katika kuimarisha stadi ya kuandika<br>e. Kuthamini utunzi wa sentensi sanifu katika mawasiliano. | • Mwanafunzi atunge sentensi zenye matumizi ya **huyu** na **hawa** k.m. Huyu anakata kucha - Hawa wanakata kucha; Huyu anachana nywele - Hawa wanachana nywele.<br>• Mwanafunzi aandike sentensi zinazojumuisha matumizi ya **huyu** na **hawa.**<br>• Mwanafunzi asome sentensi zinazojumuisha matumizi ya **huyu** na **hawa.**<br>• Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia **huyu** na **hawa.**<br>• Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwenye tarakilishi kupitia mchezo wa kuburura na kutia kapuni. | **1) Je, unajua ni kwa nini tunatumia *huyu* na *hawa*?**<br>**2) Je, utatumia neno lipi kuonyesha kwamba mtu ni mmoja?**<br>**3) Watu wakiwa wengi unaonyesha vipi?** |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
Mawasiliano na ushirikiano – mwanafunzi anashiriki katika makundi kuimba na kukariri mashairi, kusimulia na kujadiliana
Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi atajenga msingi wa kusoma na kuchunguza zaidi kuhusu usafi
Ujuzi wa kidijitali : vifaa vya teknolojia vinatumiwa katika kusimulia, kuimba na kukariri mashairi

| Ubunifu: mwanafunzi anajenga ubunifu wake anaposimulia na kutunga sentensi akitumia maneno ya vitendo. | |
|---|---|
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>Elimu ya afya - usafi wa kibinafsi<br>Wanapozingatia usafi wa mwili wao. | **Uhusiano na Maadili:**<br>Uwajibikaji. |
| **Uhusiano na Masomo mengine:** English Activities**,** Environmental Activities, Health and Nutrition na Religious Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:** kusisitiza kuhusu utunzaji wa mwili miongoni mwa wenzake<br>kulinda usiri wa mwili wake. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>kazi ya vikundi<br>shughuli za vikundi vya ushirika shuleni<br>michezo<br>nyimbo na mashairi kuhusu usafi wa mwili. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• Kuuliza maswali kuhusu jinsi ya kuzingatia usafi wa mwili<br>• Kuchunguza anavyotamka sauti zilizofunzwa<br>• Kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa<br>• Kuchunguza jinsi anavyotumia **huyu** na **hawa** katika sentensi. |

## Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|
| **Mwanafunzi,**<br>• Anatamka sauti lengwa kwa ufasaha<br>• Anaelezea jinsi ya kuzingatia usafi wa mwili kwa ufasaha<br>• Anatumia msamiati wa usafi wa mwili kwa ubunifu katika sentensi<br>• Anasoma kwa ufasaha<br>• Anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi | **Mwanafunzi,**<br>• Anatamka sauti lengwa vyema<br>• Anaelezea jinsi ya kuzingatia usafi wa mwili<br>• Anatumia msamiati unaotumika katika usafi wa mwili ifaavyo katika sentensi.<br>• Anasoma ifaavyo<br>• Anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na | **Mwanafunzi,**<br>• Ana changamoto za kutamka baadhi ya sauti lengwa vyema<br>• Anaelezea jinsi ya kuzingatia usafi wa mwili<br>• Ana changamoto za kutumia baadhi ya misamiati ya usafi wa mwili ifaavyo katika sentensi<br>• Anasoma baadhi ya kazi anazopewa<br>• Anajibu baadhi ya maswali ya | **Mwanafunzi,**<br>• Ana changamoto za kutamka sauti lengwa vyema<br>• Ana changamoto za kuelezea jinsi ya kuzingatia usafi wa mwili<br>• Ana changamoto za kutumia msamiati usafi wa mwili ifaavyo katika sentensi<br>• Ana changamoto katika kusoma<br>• Ana changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| • Anatumia *huyu* na *hawa* kutunga sentensi kwa ubunifu<br>• Anaandika kwa hati nadhifu**.** | masimulizi kwa usahihi<br>• Anatumia *huyu* na *hawa* kutunga sentensi ifaavyo<br>• Anaandika kwa hati bora. | ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi<br>• Ana changamoto za kutumia umoja na wingi wa majina lengwa katika kutunga sentensi<br>• Anaandika kwa hati zinazosomeka. | • Ana changamoto katika kutumia umoja na wingi wa majina lengwa katika kutunga sentensi<br>• Ana changamoto katika kuandika. |

| MADA | MADA NDOGO | MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MASWALI DADISI |
|---|---|---|---|---|
| **Vyakula vya kiasilia** | Sauti na majina ya herufi za Kiswahili (Vipindi 8) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kutamka sauti nne za herufi moja katika kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>b. Kutambua sauti za herufi moja zilizofunzwa katika maneno katika kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>c. Kutambua majina ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>d. Kusoma herufi za sauti moja katika kuimarisha stadi ya | • Mwanafunzi atambue sauti lengwa /s/, /b/, /y/ na /z/ katika maneno.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu akitamka sauti lengwa, kisha atamke pamoja na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake, wawili na kama darasa.<br>• Mwanafunzi atumie teknolojia (papaya) kutamkia sauti.<br>• Mwanafunzi atambue herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi.<br>• Mwanafunzi aambatanishe silabi kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi atenganishe silabi katika kutambua sehemu mbalimbali za maneno.<br>• Wanafunzi waweza kushirikishwa kusikiliza mgeni | **1) Ni sauti zipi unazoweza kutamka?**<br>**2) Unajua kusoma herufi na maneno yapi?**<br>**3) Unajua kuandika herufi na maneno yapi?** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kusoma<br>e. Kusoma maneno kwa kutumia silabi zinazotokana na sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>f. Kusoma vifungu vilivyo na maneno yaliyo na sauti lengwa katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>g. Kuandika maumbo ya herufi yanayowakilisha sauti lengwa<br>h. Katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>i. Kuchangamkia kutumia maneno yanayojumuisha sauti lengwa katika mawasiliano ya kila siku. | mwalikwa mwenye umahiri wa kutamka sauti lengwa.<br>• Mwanafunzi aweza kufinyanga maumbo ya herufi inayowakilisha sauti iliyofunzwa.<br>• Mwanafunzi aandike maumbo ya herufi za sauti alizosoma hewani na vitabuni.<br>• Mwanafunzi asome maneno kwa kutumia silabi au kwa kugawa maneno marefu katika sehemu ndogo ndogo ili kuyasoma kwa urahisi.<br>• Wanafunzi wasome hadithi zilizo na maneno yanayobeba sauti lengwa kama darasa au wawili wawili.<br>• Mwanafunzi anaweza kushirikishwa kusikiliza na kusoma hadithi kupitia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta n.k.<br>• Mwanafunzi ashirikishwe katika kuandika imla ya maneno yaliyo na herufi za sauti alizofunzwa na kuyaandika. | |
| | Msamiati (Vipindi 2) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br><br>a. Kutambua vyakula vya kiasili ili kuimarisha lishe bora<br>b. Kusoma majina ya vyakula mbalimbali ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>c. Kuandika majina ya vyakula katika kuimarisha stadi ya kuandika<br>d. Kutumia majina ya vyakula | • Mwanafunzi atambue vyakula mbalimbali vya kiasili kwa kutumia vyakula halisi, picha na michoro kama vile mihogo, viazi, mahindi , maharagwe, mboga na matunda.<br>• Mwanafunzi atumie msamiati aliyofunzwa kutunga sentensi.<br>• Mwanafunzi aandike maneno aliofunzwa.<br>• Mwanafunzi aweza kupewa kadi za majina ya vyakula vya kiasili asome kwa sauti.<br>• Wanafunzi waweza kuambatanisha majina ya vyakula halisi au michoro na majina yavyo. | **1) Unapenda waweza kutaja chakula kipi?**<br>**2) Vyakula vipi hukuzwa shambani?** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | katika sentensi sahihi<br>e. Kuthamini vyakula vya kiasili katika maisha ya kila siku. | • Wanafunzi waweza kuimba nyimbo na kukariri mashairi kuhusu vyakula vya kiasili.<br>• Wanafunzi waweza kuandika majina ya vyakula wanavyovijua katika vikundi.<br>• Wanafunzi waweza kutazama picha za vyakula mbalimbali kupitia kwa vifaa vya kiteknolojia. | |
| | Kusikiliza na Kuzungumza: Masimulizi (Vipindi 2) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kusikiliza masimulizi kuhusu vyakula vya kiasili katika kuimarisha stadi ya kusikiliza<br>b. Kusimulia visa vinavyohusu<br>c. Vyakula vya kiasili katika kuimarisha stadi ya kuzungumza<br>d. Kufahamu masimulizi aliyosikiliza katika kuimarisha stadi ya kusikiliza<br>e. Kufurahia vyakula vya kiasili katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi asimulie hadithi kuhusu vyakula vya kiasili.<br>• Wanafunzi wajadiliane kuhusu umuhimu wa vyakula vya kiasili.<br>• Wanafunzi wasimuliane visa kuhusu vyakula vya kiasili.<br>• Mtaalamu wa lishe bora aweza kualikwa kuzungumzia juu ya vyakula vya kiasili.<br>• Mwanafunzi aulize na kujibu maswali kutokana na maelezo aliyosikia kuhusu vyakula vya kiasili.<br>• Mwanafunzi aweza kuhusishwa katika kuimba nyimbo na kukariri mashairi kuhusu vyakula vya kiasili.<br>• Mwanafunzi aweza kusikiliza nyimbo na mashairi yaliyorekodiwa kwenye vifaa vya kiteknolojia kuhusu vyakula vya kiasili. | **1) Kwa nini tunakula chakula?**<br>**2) Je, umuhimu wa vyakula vya kiasili ni upi?** |
| | Kusoma: Hadithi (Vipindi 3) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br>a. Kutambua msamiati uliotumiwa katika hadithi aliyosoma au kusomewa ili kuimarisha | • Mwanafunzi ajadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi atabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi afahamu matumizi ya msamiati | **1) Je, unaona nini katika picha?**<br>**2) Unadhani ni nini kitakachotokea** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | mawasiliano<br>b. Kusikiliza hadithi zikisomwa na mwalimu kuhusu vyakula vya kiasili ili kuimarisha stadi ya kusoma<br>c. Kusoma hadithi kuhusu vyakula vya kiasili katika kuimarisha stadi ya kusoma<br>d. Kufahamu hadithi aliyosoma na kusomewa kuhusu vyakula vya kiasili ili kupata ujumbe unaolengwa<br>e. Kufurahia vyakula vya kiasili maishani. | uliotumika kwenye hadithi.<br>• Mwanafunzi asikilize mwalimu anaposoma hadithi, asome pamoja na mwalimu kisha asome peke yake, wawili wawili au katika vikundi.<br>• Mwanafunzi asikilize hadithi ya mwalimu au hadithi iliyorekodiwa kuhusu vyakula vya kiasili.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma na na kusomewa hadithi kupitia vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi, projekta n.k.<br>• Mwanafunzi aweza kusoma hadithi kwa kutumia jitabu mbele ya darasa.<br>• Mwanafunzi athibitishe utabiri wake baada ya kusoma na kusomewa hadithi.<br>• Mwanafunzi atoe muhtasari wa hadithi.<br>• Wanafunzi aulize na kujibu maswali kutokana na hadithi | **katika hadithi?**<br>**3) Unakumbuka hadithi gani uliyoisoma?** |
| | **Sarufi:**<br>Matumizi na –**angu** na –**etu**<br>(Vipindi 2) | **Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:**<br><br>a. Kutambua matumizi ya –**angu** na –**etu** katika mawasiliano<br>b. Kutumia –**angu** na – **etu** katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano<br>c. Kufurahia kutumia –**angu** na –**etu** katika mawasiliano. | • Mwanafunzi atunge sentensi zenye matumizi ya **-angu** na **–etu.**<br>• Mwanafunzi aandike sentensi zenye kuhusisha **-angu** na **–etu.**<br>• Mwanafunzi asome sentensi zenye kutumia maneno **-angu** na **–etu.**<br>• Mwanafunzi aweza kujaza mapengo kwa kutumia **-angu** na **–etu.**<br>• Mwanafunzi aweza kupewa zoezi la kujaza mapengo kwa tarakilishi (mchezo wa kuvuta na kutia kapuni). | **1) Je, ni maneno gani tunayotumia kuonyesha kuwa kitu ni chako au ni chenu?** |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – kujadili katika makundi au wawili wawili

| | |
|---|---|
| • Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi atajenga msingi wa kujua vyakula zaidi<br>• Ujuzi wa kidijitali –matumizi ya vifaa vya kiteknolojia. | |
| **Uhusiano na masuala mtambuko:**<br>Elimu ya afya: magonjwa yanayohusiana na vyakula – kuthamini vyakula vya kiasili. | **Uhusiano na Maadili:**<br>Uwajibikaji |
| **Uhusiano na Masomo mengine:**<br>Health and Nutrition Activities na Environmental Activities | **Mapendekezo ya shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji:**<br>Kuwahamasisha wengine katika jamii kuhusu umuhimu wa vyakula vya kiasili. |
| **Mapendekezo ya shughuli zingine zilizoratibiwa za ujifunzaji:**<br>• Kazi ya vikundi<br>• Michezo<br>• Nyimbo na Mashairi kuhusu usafi wa mwili. | **Mapendekezo ya Tathmini:**<br>• Kuuliza maswali kuhusu vyakula vya kiasili<br>• Kuchunguza anavyotamka sauti zilizofunzwa<br>• Kuchunguza jinsi mwanafunzi anavyojibu maswali ya masimulizi na hadithi na kutoa muhtasari wa hadithi aliyosomewa au kusimuliwa<br>• Kuchunguza jinsi anavyotumia **–angu** na **-etu** katika sentensi. |

## Viwango vya Kuzingatia katika Kutathmini

| Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| ***Mwanafunzi,*** <br>• Anatamka sauti lengwa kwa ufasaha <br>• Anaelezea mifano ya vyakula vya kiasili <br>• Anatumia msamiati wa vyakula vya kiasili kwa ubunifu katika sentensi <br>• Anasoma kwa ufasaha <br>• Anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa ubunifu na usahihi <br>• Anatumia **-angu** na **-etu** kutunga sentensi ifaavyo <br>• Anaandika kwa hati nadhifu. | ***Mwanafunzi,*** <br>• Anatamka sauti lengwa vyema <br>• Anataja mifano ya vyakula vya kiasili <br>• Anatumia msamiati wa vyakula vya kiasili ifaavyo katika sentensi <br>• Anasoma ifaavyo <br>• Anajibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi <br>• Anatumia **-angu** na **-etu** kutunga sentensi ifaavyo <br>• Anaandika kwa hati bora. | ***Mwanafunzi***, <br>• Ana changamoto za kutamka baadhi ya sauti lengwa vyema <br>• Anataja mifano ya vyakula vya kiasili <br>• Ana changamoto za kutumia baadhi ya msamiati wa vyakula vya kiasili katika sentensi <br>• Anasoma baadhi ya kazi anazopewa <br>• Anajibu baadhi ya maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi kwa usahihi <br>• Ana changamoto za kutumia **-angu** na **-etu** kutunga sentensi ifaavyo <br>• Ana changamoto katika kusoma. | ***Mwanafunzi,*** <br>• Ana changamoto za kutamka sauti lengwa vyema <br>• Ana changamoto za kutaja mifano ya vyakula vya kiasili <br>• Ana changamoto za kutumia msamiati wa vyakula vya kiasili katika sentensi <br>• Ana changamoto katika kusoma <br>• Ana changamoto katika kujibu maswali ya ufahamu katika hadithi na masimulizi <br>• Ana changamoto za kutumia **-angu** na **-etu** kutunga sentensi ifaavyo <br>• Ana changamoto katika kuandika. |